

REPUBLIC OF KENYA
COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THE HANSARD

Monday, 21st March, 2018

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 2:30 p.m.*

(The Deputy Speaker (Hon. Kenga) in the Chair)

PRAYERS

STATEMENTS

**ORDER OF BUSINESS FOR THE WEEK
COMMENCING MONDAY, 26TH MARCH, 2018**

Hon. (Ms) Sidi: Thank you Mr. Speaker, Sir. Pursuant to the provision of Standing Order No. 41(1) (a), I beg to move a Statement regarding the business of the House for the week commencing Monday, 26th March, 2018:-

Monday, 26th March, 2018, from 2.30 p.m. the business of the day will be; Statements; first Statement is sought by hon. Stanley Karisa from the County Executive Committee Member in charge of the Department of Agriculture, Livestock Development and Fisheries.

Next is a Statement sought by hon. Peter Ziro from the County Executive Committee Member in charge of the Department of Education and ICT. Next is a Statement sought by hon. Christopher Mwambire from the County Executive Member in charge of the Department of Health Services.

Tuesday, 27th March, 2018, from 9.30 a.m. the business of the day will be (A) Statements; first Statement will be sought by hon. Christopher Mwambire from the County Executive Committee Member in charge of the Department of Health Services. Next Statement is sought by hon. Christopher Mwambire from the County Executive Committee Member in charge of the Department of Trade, Tourism and Cooperative Development. (B), we have The Kilifi County Ward Scholarship fund Bill, First Reading.

Tuesday, 27th March, 2018, from 2.30 p.m. we have Statements; the first Statements is sought by hon. Christopher Mwambire from the County Executive Committee Member in charge of the Department of Trade, Tourism and Cooperative Development. Next is a Response to a Statement sought by hon. George Baya from the County Executive Committee Member in charge of Health Services.

Wednesday, 28th March, 2018, from 2.30 p.m. the business of the day will be Statements; first Statement it is a Statement sought by hon. Christopher Mwambire from the County Executive Committee Member in charge of Transport and Public Works. Next is a Statement

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

sought by hon. Christopher Mwambire from the County Executive Committee Member in charge of Lands, Energy, Housing and Urban Development. Last Statement is sought by hon. Christopher Mwambire from the County Executive Committee Member in charge of Lands, Energy, Housing and Urban Development.

That is the programme for the week. Thank you, Mr. Speaker.

MOTION

DEVELOPMENT OF A SPORTS ACADEMY AT BOMANI, MAGARINI WARD

Hon. Hadad: Motion to the County Executive Committee Member in charge of Gender, Social Services, Culture and Sports. I beg to move:-

THAT, aware that the Fourth Schedule Part II of the Constitution of Kenya, 2010, empowers counties to develop sports, cultural activities and facilities.

FURTHER AWARE THAT, sports activities have unique powers to attract, mobilize, inspire, empower and create employment opportunities for the youth as well as being a high impact tool in creating positive alternatives to youth anti-social behavior and crime.

COGNIZANT OF THE FACT THAT, the Bomani community in Magarini Ward has available land with an approximated coverage of 25 acres that can be used for the establishment of a Sports Academy to tap talents among the youth of Kilifi County.

This House urges the County Executive Committee Member in charge of Gender, Social Services, Culture and Sports to allocate funds for the establishment and development of a County Sports Academy at Bomani in Magarini Ward in the Financial year 2018/2019.

I would like hon. Abdulrahman Omar to second.

The Deputy Speaker (Hon.) Kenga: Just before hon. Abdulrahman Omar, you could move ahead and make your contribution regarding the same.

Hon. Hadad: I would like to say that for one to start a business, you must have resources available. You cannot start any type of business without the availability of the recourses required for such a business to take place and for me to point out the sports area to be in Magarini Ward at Bomani, is because the land is available thus we have cut down the expenses of purchasing the land given out by the community; in fact, it has a title deed.

So for me, I suggested this place, Bomani, because of factor number one; availability of land which has less expenses to us. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon.Kenga): Yes, who is seconding?

Hon. Hadad: Hon. Abdulrahman Omar.

The Deputy Speaker (Hon.) Kenga: Yes Proceed. There is an intervention from hon. Mwarandu.

Hon. Mwarandu: Naomba aongee kwanza mimi nitaongea...

The Deputy Speaker (Hon.) Kenga: Okay, you wanted to contribute? It was not on a point of Order?

Hon. Mwarandu: Yeah.

The Deputy Speaker (Hon.) Kenga: Okay thank you. Please proceed.

Hon. Omar: Thank you Mr. Speaker. There is no objection on that issue only that I support the Motion. Thank you, Mr. Speaker.

(Hon. Omar seconded)

Disclaimer: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.

(Question proposed)

Hon. Mwarandu: Asante sana mheshimiwa Spika. Nimesimama kupinga Hoja hii na nina sababu za kuipinga. Kwanza kabisa, nataka nielewe fika kwamba mwenye ameleta hoja hii labda hajui maana ya *Sports Academy* ama awe alishauriwa vibaya. Maana ya *Sports Academy* ni kwamba ni pahali ambapo watoto huenda wakapata mafundisho aidha ya kimchezo ili kukuza vipaji vyao na kuifanya kama kazi ya mapato mbeleni. Tunaongelea kina nani? Tunaongea kuhusu watoto.

Mheshimiwa Spika, aliyeleta Hoja hii kiegozo chake ni kimoja kwa sababu kuna ardhi tayari imewekwa ndio maana huu mfumo unaweza kupelekwa Magarini lakini je, alifanya utafiti kujua ni watu wangapi wana mvuto wa *Sports Academy*? Ina maana kwamba tunaweza kupeleka kitu pahali ambapo hakihitajiki ama watu hawajakuwa tayari nacho. Tunataka tutetee pesa maana kujenga *Sports Academy* itatugharimu sio chini ya shilingi milioni mia tano. Je, pesa hizi tukiziekeza mahali ambapo watu hawana mvuto wa hilo jambo, tutakuwa tumeziharibu au la?

Kuna maswala mengi ambayo mtu lazima ayaweke maanani kabla aseme kwamba *Sports Academy* iende mahali fulani. Kuna mfano ambao uko hapa Mnarani; sio wa serikali ni wa kibinafsi, unaitwa *Moving the Goal Post*. Mfano huu tumeona unaendeleza vipaji vya watoto wa kike, na anayevaa jezi namba tisa wa hiyo timu ya Harambee Starlets, Tisi Akida, alitoka pale. Walipoanzisha, walifanya utafiti na wakaona afadhali waweke maeneo yale; walianza na shule tatu za karibu na pale. Ukumbuke kwamba ukiweka jengo hilo sio kwamba watu kutoka sehemu nyingine watakuja. Wataanza na watu wa pale mwanzo, kama watu wa pale hawana mvuto, jengo hili litaendelea kutumika ipaswavyo? Ijapokuwa Hoja hii ni nzuri, lakini mwenye kuileta hakutaka kwanza kufanya utafiti na vigezo gani ambavyo vinapaswa viwekwe ili kudumisha hii *Sports Academy*.

Swala la ardhi ni la mwisho kabisa. Kuna vigezo vingine kama ufikaji wa pale mahali, hali ya usalama, maanake unaweka pesa mahali ambapo pengine hakuna usalama. Nataka aidha mwenye Hoja hii aiondoe ili akaitunge tena na kabla kuitunga kwanza, afanye utafiti, maanake pia lazima tupeleke kitu mahali ambapo kinatakikana. Hii ni sawa na kuza mahamri siku ya sikukuu. Naonelea Hoja hii waheshimiwa wenzangu wenye fikra za kusaidia pesa na sio pesa kidogo pesa zaidi ya shilingi milioni mia tano kwenda mpaka bilioni moja kupotea ama kutumika vibaya. Ni bora tuipingie ama tumpe fursa mwenye kuleta Hoja hii kuitunga tena na kabla ya kuileta pia afanye utafiti ni maeneo gani jambo hili lina mvuto licha ya kuwa kuna ardhi. Kwangu mimi, naomba waheshimiwa waipingie mpaka vigezo hivi vingine vifwatiliziwe.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): There is an intervention from Hon. Hadad.

Hon. Hadad: Napendelea kumuuliza swala dogo sana, ukitaka kujenga nyumba ya mawe unaenda mahali mawe yanatolewa ama unatumana yanaletwa ndio unajenga nyumba yako? Kufwatilia maswala hayo mengi, *Sports Academy* ni kitu nilikuwa nikiwazia na kufwatilia na niko na ufahamu ya elimu ya michezo ni nini. Sijaleta Mswada *with a blind eye*; nimeileta kwa sababu naelewa nafanya nini. Hii *Sports Academy*. Ikianza mahali mwanzo inasaidia kazi kwa wananchi na pili inasaidia eneo kukua ki miundo msingi.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Member, because you had already gotten the opportunity to make your contribution, please take your seat. I will direct that before I put the Question, you will have an opportunity to address all the concerns and questions that will have been raised by the Members who are making contributions. Kindly please reserve your submissions. There was a request from hon. Jana. Please proceed.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Jana: Asante sana Bw. Spika nimesimama kuunga mkono Hoja hii. *Sports Academy* ni kitu ambacho ni muhimu sana kwa vijana wetu wa karne hizi. Nikisema hivyo ni kwamba nchi za kigeni watu wameendelea kupitia mambo kama haya. Mzungumzaji aliyepinga Hoja hii ni kwamba analalamikia akisema kwamba hizo pesa sio za mamake...

(Laughter)

Nasema kwamba hata sio Magarini peke yake tunaomba kila eneo bunge katika Kaunti ya Kilifi liwe na mradi kama huu. Kwa hayo ninaunga mkono Hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Asante Bw. Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Before you take your seat, there is an intervention from hon. Mwarandu.

Hon. Mwarandu: Mheshimiwa Spika, kusema kweli, hizi pesa sio za mamangu na hilo ni kweli lakini ajue mamangu pia anatoa ushuru na mimi mwenyewe natoa ushuru. Hizo pesa sio za mamangu ni za mwananchi yeyote yule hata mamake ...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Is it a point of information or order?

Hon. Mwarandu: Point of order. Bunge hili ni la heshima ndio maana linakaa waheshimiwa. Akina mama zetu ni watajwe na mambo ambayo ni sahihi kwa sababu vile alivyoongea Mheshimiwa Jana ni kama tusi alilolielekeza kwangu. Naomba Mheshimiwa Jana alifute na kuliondoa katika sakafu ya Bunge hili, ili niwe nami niko radhi na mamangu pale alipo pia atakuwa yuko radhi. Nahisi mamangu ametusiwa katika Bunge la heshima. Sio bora kamwe kwa mheshimiwa ambaye nina mheshimu aongee maneno kama hayo.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes proceed.

Hon. Jana: Asante naomba kuliondoa.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Mheshimiwa Elina.

Hon. (Ms.) Elina: Asante sana mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi niweze kuchangia mjadala ambao uko mbele yetu. Naunga mkono Mswada ulioletwa na Mwenyekiti mdogo wa Kamati ya Michezo. Kila kitu lazima kiwe na chanzo. Magarini tulikuwa tumepanga uwanja usio pungua ekari 25. Pale mahali tulikuwa tumepanga pawe pa michezo kwa sababu ya vijana wetu ambao wameingilia madawa ya kulevya. Kama alivyosema, anataka tuianzishe ili iweze kusaidia vijana ambao hawajabahatika kuajiriwa ili waweze kujajiri wenyewe pale mahali.

Tuko na wasanii na wacheza mpira wengi Magarini lakini hawakuwa na uwanja. Tulipokaa kwa Kamati, tukasema kile kidogo ambacho tuko nacho ingekuwa vyema tustawishe hicho kwanza; baadaye tuangalie kila eneo Bunge tuweke uwanja kama ule. Vijana walioinukia ni wengi na idadi inaendelea kuongezeka na kama tutakaa bila kuangalia hivi viwanja, kutakuwa hakuna viwanja ndio maana mheshimiwa Hadad ameonelea alete huu Mjadala.

Kaunti ya Kilifi hatuna uwanja hata mmoja mahali popote kwenye michezo ya watoto wetu. Tunaelekea wapi? Ndio tukaona tuunge mkono huu mjadala ili kuanzisha ule uwanja iwe ni chanzo kwa sababu kama alivyozungumza, huo uwanja umeshatolewa cheti cha umiliki kwamba ni uwanja wa michezo kwa hivyo ni mali ya serikali...

(Hon. Mwarandu stood on a Point of Information)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): There is a point of order from hon. Mwarandu.

Hon. Mwarandu: Mheshimiwa Spika, ningepomba nimfahamishe kwamba...

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): You raising a point of information, hon. (Ms.) Elina, would you wish to be informed by hon. Mwarandu?

Hon. (Ms.) Elina: No!

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes, proceed.

Hon. Mwarandu: Nilikuwa bado nasema, kufahamisha na ...

Hon. (Ms.) Elina: Sitaki kufahamishwa.

Hon. Mwarandu: Si kwamba nilikuwa nataka kumfahamisha vile, bali nataka...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Member, hon. (Ms.) Elina is not ready to be informed, so please take your seat.

Hon. Mwarandu: Na vile ambavyo hataki kufahamishwa anapoteza wananchi wa Kilifi.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Please take your seat.

Hon. (Ms.) Elina: Kwa hivyo, nimesimama kuunga mkono hili jambo kabisa. Tuko na mahali pa vijana wetu kujinufaisha kwa kila aina ya michezo kwa sababu hizo ekari ishirini na tano (25) si shamba ndogo ambalo watoto hawawezi kutoshea pale. Kamati iko wazi, tungeweze kupeleka huu mradi hata Mnarani hatujakataa, ndio nawaomba waheshimiwa katika wadi zenu mahali ambapo unaona tunaweza kufanya uwanja mkubwa ili kusaidia wale vijana itakuwa ni vizuri tukiungana na Kamati yetu ya michezo. Sisi kama wana kamati wa ile Kamati ya Michezo, tunaona afadhali tuangalie mbele kwa sababu katika Kaunti yetu ya Kilifi, mashamba yanaisha. Kwa hivyo, naunga mkono na itakuwa ni vizuri tukiungana na Kamati yetu ya michezo, ili hili jambo liweze kufaulu ili vijana wetu waweze kuwa na uwanja wa kusherehekea katika Kaunti yetu ya Kilifi.

Vijana wengi saa hii ni wasanii na hata waheshimiwa wengine tuko nao hapa ni wakereketwa wa usanii na ningeliomba tuungane pamoja kwa sababu pale mahali pakifunguliwa patasaidia vijana wengi wa Kilifi Kaunti. Naunga mkono Bw. Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you very much hon. (Ms.) Elina. There is a request from hon. (Ms.) Mbuche, please proceed.

Hon. (Ms.) Mbuche: Asante mheshimiwa Spika. Nimesimama kama mkereketwa, msanii na naunga mkono kwa mbwembwe kabisa hoja hii ya mheshimiwa Hadad na naomba pia waheshimiwa wengine ambao pia ni wakereketwa na bado wana nguvu za kuingia viwanjani na kuonyesha mambo; tuunge mkono kwa dhati kabisa. Niko na hoja mbili ama tatu; la kwanza, uwanja huu utatusaidia na kwa kimombo tutaita *'role model'* kwa sababu tukianzia pale ndio tutafungua njia nyingi zaidi za kuzindua vipawa mbalimbali ambavyo vimefichika kwa sababu mwanzilishi ndio kulikuwa hakuna. Nashukuru mimi pia ni mwanachama wa Kamati hii ya michezo na tulikuwa pamoja na mheshimiwa Hadad pamoja na wanachama wengine na tukasema hapa ni kwetu na kuna karatasi ya umiliki tuanzie hapa ili tufungue kwengine hapo mbeleni.

Pili ni kwamba, mimi kama msanii nimeanza mikakati kule Kilifi. Huwa nafuata sana kule nyumbani kwa sababu huniona kwa televisheni na huwa wanatamani wafike pale nimefika. Ina nipa shida kwa sababu nauzia sanaa yangu Kaunti ya Mombasa. Nimejaribu sana na waheshimiwa wengine pia wamefatwa na wasanii kadhaa ili wawasaidie. Tumepewa majukumu ya kulea hawa vijana na talanta zao ili tuwasaidie wasongee.

Tuunge mkono hoja hii ili talanta hizi ziweze kutumika na kusaidia wale vijana wawe raia wema na wajenge gatu letu la Kilifi na tuendele mbele. Natamani huu uwanja uzinduliwe hata kesho kwa sababu tuko na vijana elfu tano huwa nakutana nao, nimekuwa na mikutano kadhaa. Tumepata uwanja mdogo pale Kilifi, unaitwa *"Youth Empowerment Centre"* ...

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Hon. Mwarandu stood on a Point of Order)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): There is a point of order from hon. Mwarandu.

Hon. (Ms.) Mbuhe: Naomba kumaliza hoja yangu ya mwisho halafu aendelee...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Member, please take your seat so that he can raise his point of order.

Hon. Mwarandu: Mheshimiwa Spika, naona kuna waheshimiwa wanataka kupotosha hili Bunge. Hapa tunaongelea uwanja ama tunaongelea *kuhusu academy? Academy* mara nyingi ni watoto wanaoenda huko si watu wazima. Uwanja unaweza kuwa popote, hii ni *academy* mheshimiwa Spika. Kwa hivyo, waheshimiwa wakisimama na kusema...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Are you on a point of order or point of information? You are making contributions yet you have already had your time to make contributions.

Hon. Mwarandu: Mheshimiwa Spika, mimi nikiona mtu anapotosha watu nasikia kuumia kwa hivyo ...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): But give them an opportunity to make their contributions. At the end of the day, I am going to put the Question depending on how they have been convinced, they will either support or abort the Motion ...

Hon. Mwarandu: Mheshimiwa Spika, hawawezi endelea kupotosha watu...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes but you are rising on a point of order and it is information you are giving. Please take your seat. Hon. (Ms.) Mbuhe please proceed.

Hon. (Ms.) Mbuhe: Asante sana mheshimiwa Spika. Nilikuwa nasema Kilifi tulipatiwa mahali padogo panaitwa *Kilifi Empowerment Centre*. Hapa mahali pako chini ya Serikali ya Kitaifa, na kulipeanwa kitambo kwa vijana lakini kuna watu walikuwa ni kama wamepamiliki. Vijana wa ngazi zote walishikana juzi; wengine wamebobeza na hawajui watauzia wapi talanta zao na wengine hawajui hata kama wanaweza kupata pesa kupitia talanta zao. Sio ati vijana peke yake bali kuna hata watu wazima ambao ni *sports men* na *sports ladies* na wanaweza kuwa walimu lakini hili zoezi litafanyika wapi? Hakuna mahali ama nyumba moja ambayo tunaweza kuwapeleka wasanii wengi ambao tayari tuko nao.

Kwa hivyo, kuna wachache ambao wamejikusanya katika *empowerment centre* na hata kesho tunakutana na Waziri kusaidia tutafanya vipi na Waziri ameshauriwa kuona ni wapi tunaweza anzia. Naomba Bw. Spika, pamoja na waheshimiwa wenzangu mlio hapa; tukizungumza hii Hoja ya sanaa ni kubwa maana hata wengi hapa najua nyinyi ni wasanii na mnapenda sanaa; inanzia *sports dance* na kila kitu. Naomba tuunge mkono huu uwanja uzinduliwe rasmi tuanze mikakati ya kutengeneza hizo *academies* na kila kitu maana kutokana na hiyo tutaweza kutengeneza kazi nyingi sana za wasanii, wanaspoti na kila mtu atahusika kujenga taifa kupitia kwa nguvu zetu sisi wanasiasa ambao tutakuwa tumeunga mkono.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you hon. Member for your contributions. There is request form hon. Ziro, please proceed.

Hon. Ziro: Asante sana Mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono Hoja hii. Kwanza, nataka kumshukuru Mheshimiwa ambaye ameenda akafikiria na kuja na mjadala huu ili tuweze kuujadili na hatimaye tuupitishie ili kwamba Inshallah kwa majaliwa ya Mwenyezi Mungu *Subhānahu wa ta'alā* tuwe na kiwanja cha watoto wetu kuweza kuwapa mafunzo ambayo yatawasaidia katika maisha yao.

Nikiongezea ni kwamba mradi huu ushaanza kwa sababu tuko na kiwanja na *title deed* kwa hivyo pesa za umma tayari zishatumika. Kusema ati mradi huu usiendelee ni kumaanisha wewe hujali hii Kaunti ya Kilifi na unataka watu wa Kilifi waendelee kugandamizwa kwa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

sababu pesa tayari zishatumika na mradi umeanza. Ukisema usiendelee basi naona hapo utakuwa umekosa mwelekeo.

Jambo bora ni watu kuunga mkono huu mswaada kwamba huu mradi uzidi kuendelea ili vijana wetu wapate mahali pa kujifundisha talanta zao kama vile Mheshimiwa Mbuche alivyozungumza kwamba kuna vijana, hata watu wazima, hata mimi mwenyewe ni mchezaji wa kandanda na sasa hivi ninavyokwambia, Mheshimiwa Spika, sina kiwanja ambacho naweza kuenda kucheza. Mradi huu ukianza, utakuwa unanipa fursa na mimi kwa sababu niko karibu kule Magarini naweza kwenda siku moja nikajivinjari na kucheza na wale vijana.

Huu mradi ukianza, utasaidia vijana wetu wanaojiingiza katika dawa za kulevya kule nyanjani kwa kukosa kazi. Watakuwa na wakati mzuri wa kuenda pale na kujifundisha na vile vile itapunguza hata idadi ya wasichana wetu ambao wanaingizwa mimba na vijana hawa ambao hawana kazi ya kufanya. Vijana wakiwa na kazi ya kufanya na wakichoka jioni kama tunavyojua sote wanaume ukifika umechoka nyumbani utalala, lakini kama umeshinda bila kazi yoyote na ule vizuri jioni ikifika damu yaenda mbio; ndio unakuta kuna watu wanatoka sehemu za Kakuyuni hutembea usiku wakiangalia wasichana wa watu. Mheshimiwa Spika, naunga mkono huu Mswaada mia kwa mia tuupitishhe.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga) Thank you hon. Member for you contributions. Hon. Ms. Victoria, please proceed.

Hon. (Ms.) Victoria: Asante sana Bw. Spika. Naitwa hon. Mazungu. Kwanza, naunga mkono Hoja hii lakini kabla ya kutoa changizo zangu, nina hofu na wasiwasi kama sote tuko timamu hapa kama waheshimiwa. Kama unaweza kupinga maendeleo ya Kilifi, basi kuna kitu ambacho hakiko sawa ama stakabadhi zetu sio za nchi hii ya Kenya. Ninaomba tufanyiwe uchunguzi stakabadhi zetu na pia tuchunguzwe kiakili pengine kuna hitilafu fulani maanake sioni vipi mkaazi wa Kilifi anaweza kupinga jambo kama hilo...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): There is a point of order from hon. Mramba. Take your seat and give an opportunity to hon. Mramba to proceed.

Hon. Mramba: Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Hoja ya nidhamu. Mheshimiwa anayeongea kwa sasa naona amevuka mipaka kusema kwamba kuna wengine labda akili zao si timamu. Huu ni mdahalo na haijaandikwa kwamba lazima Mheshimiwa aunge mkono au akatae. Kila mmoja anaweza kuongea maoni yake kisha halafu wengi watapitisha. Kwa hivyo, sidhani kama kuna mtu yoyote ambaye ana hitilafu bali ni uhuru wa kila mmoja wa kuongea kile anataka...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Please hon. Member, apologize and withdraw.

Hon. (Ms.) Victoria: Before I apologize, I think he has suspected himself but I apologize. Naunga mkono Hoja hii na naomba tukubaliane kwamba hakuna sehemu yoyote ambayo haina watoto. Swala lolote linalolenga mtoto hata likawekwa wapi bado litafanya kazi kwa sababu kila mahali kuna watoto tena kwa idadi kubwa. Kwa hivyo, hata huko Magarini hilo jengo likiwekwa huko, bado litakuwa na manufaa na sio lazima watu watoke Magarini watu watasafiri ndani ya Kaunti yetu. Hata shule zikifungwa ama kufunguliwa, watoto tunawasafirisha kwenda au kutoka shuleni, hata huko itakuwa hivyo hivyo.

Hiyo isiwe sababu ya kupinga huo mradi kuendelezwa maana itakuwa ni kama tunajirudisha nyuma. Jambo limeshaanza; tuanze tena kutafuta uwanja mahali kwengine na hatimaye ule uwanja utapotea. Hapo ndio sisi tutakuja hapa tena kupiga kelele kiwanja kimechukuliwa na mabwenyenye ilhali hapa uwanja uko tayari kwa manufaa yetu na watoto wetu. Hakuna vile ambavyo ile *academy* ikiwekwa pale itakosa watoto. Watoto ndani ya kaunti watasafiri kuifwata hiyo *academy* pale ilipo na watoto watasaidika. Ninaomba jambo hili

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

tuliunge mkono mia kwa mia tusonge mbele tuangalie mambo mengine. Hili jambo liwe hata maeneo mengine sio Magarini peke yake.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga) Hon. (Ms.) Scholastica.

Hon. (Ms.) Scholastica: Thank you Mr. Speaker. I stand to support this Motion. First, I would really like to appreciate hon. Hadad for bringing this Motion to this House. Actually, this Motion is very important especially for Kilifi County. As we see, most of our youth are really talented but they have nowhere to come together and practice. We have so many youth engaging in drugs and prostitution for the ladies who are idle, some of them as we know in Kilifi County. I am sorry to say this; educationally we are a bit down. After form four or class eight, some drop out at class eight and some do not perform so well in form four but at least they are talented.

Now, for such youths, where are we going to take them? If we are really going to say that we are not going to have Sports Academy centers in Kilifi County, where are we going to take our boys and girls? We know a place in Malindi called Lamu Road. It does not matter whether they are coming from Kilifi County or upcountry. Once they come here and they find that no one is going to Lamu Road because we have a place where these youth can come and do something productive, actually we are going to remove the ladies from Lamu Road because once they come to Malindi, instead of a night of prostitution it will be a night for doing something very productive in some of our halls in Malindi.

Secondly, we know we have many talents in Coast; we have acrobatics and the rest. All these talents can be done if we have a place to harbour these children. Hon. Humphrey Mwarandu was talking about an academy for the kids yes; it is not a problem even the young kids have talent.

I was once a nursery school teacher and you can see and tell who has a talent and they can travel from all over the county. Magarini is far and also that is going to encourage parents who are not from Magarini whenever we close schools, we will be organizing for our kids to go there to have lessons and stay there for a week or two because it is also a way of kids coming together and realizing their talents while sharing ideas and once they go back to their places, at least they will have something additional to what they know.

We know we have very remote areas in Kilifi County like Chakama; you get a child from Chakama he has a talent and he cannot express himself or speak well but he knows how to act and once you take them there, if we have an academy, at least that child will come out with something to go back to Chakama and influence the other kids.

About development; do you want Magarini to remain the way it is? We want Magarini to be like Malindi Town. So in one way, we are going to bring development to that area and we will even have people coming from all over the country and it will be known hence the place will be developed. We shall create jobs for our youth so that they may not engage themselves in drugs. Drugs is really on the high side so in one way, our youths are going to be engaged there. They will have good manners and I believe we are going to take Kilifi from one place to another.

Immorality is going to go down completely trust me because immorality starts with the youths and as the hon. Member had said, if they are busy they will forget about this because after struggling the whole day, they will not think of anything. They will just think of sleeping and nothing else but once their minds are idle, I am telling you, they will do the worst. So this is the best place. I really support and I would beg to sit down Mr. Speaker. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you for making your contribution. Hon. (Ms) Kalume (Carol) please proceed.

Disclaimer: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.

Hon. (Ms.) Carol: Thank you very much Mr. Speaker. I stand to partially oppose this Motion reasons being that I feel there is need for proper research to be done so that when we come to discuss further, let us have on paper a survey or a research that will give us confidence that it is high time to come up with such an academy.

Also Mr. Speaker, Sir, an academy is a place where youths go to learn the right techniques and tactics to prepare them for professional careers. Most young people enroll in the academy for one reason to learn and to become world class professionals. However, setting up an academy gives us an opportunity to do more than just teach the youth skills. You can also create and organize a safe environment to nurture the social and moral values of the young people in Kilifi. Setting up of this academy is a daunting and a challenging task; one that should not be taken lightly without doing proper research and survey.

Mr. Speaker, Sir I stand to oppose this Motion up to the moment proper research and survey is done so that we are given confident information and we do not lose any resources and monies in such a project. Thank you very much.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you very much, the hon. Member for Mwawesa Ward for making your contributions. Hon. Changawa, did you want to make contributions? I am not getting any request from hon. Members and I do not want to lock Members out. For those who would wish to make contributions, please you tap the intervention button. Hon. Kadenge please proceed.

Hon. Kadenge: Asante Bw. Spika. Pia mimi nasimama kwa hoja ya kuunga mkono Hoja ambayo imeletwa na kijana mwenzetu ambaye ni mheshimiwa Hadad. Nafikiri tukiangalia maisha ya watoto wetu hasa wale wa mjini...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes, hon. Mramba what is your point of order?

Hon. Mramba: Hon. Kadenge Dadu is implying that the Motion has been brought by our fellow youth yet I know very well that Kadenge Dadu is past the age of youth. Can he please confirm his age because when he says “imeletwa na kijana mwenzetu” and I know very well that he has passed the age of youth, Mr. Speaker.

(Laughter)

Hon. Kadenge: Asante Bw. Spika. Mimi nina miaka ishirini na tatu (23) na ninaona niko karibu sana na kijana ambaye ameleta hoja hii. Wacha niendeleo kuunga mkono hii hoja ambayo iko mbele yetu...

Hon. Ziro: Point of order Mr. Speaker!

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): You have not made your intervention? How then do we proceed... but I cannot...

Hon. Ziro: Mr. Speaker, I think it is not proper for the hon. Member to mislead this House. He is telling us he is 22 or 23 years, can he confirm with his identity card that he is really 23 years old or he tells us his right age?

Hon. Kadenge: Asante Bw Spika, lakini kwa sababu sikubeba kitambulisho, nafikiri Jumatatu nitaleta kitambulisho na nitawasilisha kwa mheshimiwa kujua umri wangu.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes, hon. Changawa, do you have an intervention? Yes Mwarandu.

Hon. Mwarandu: Tunajua pengine hajabeba kitambulisho lakini tunajua ofisi ya *Human Resources* iko hapa na stakabadhi zake zote ziko hapa tungeomba pengine kuletwe makaratasi yake maanake yapo ili tuje tuangalie umri wake. Kwa sababu si vizuri kudanganya nyumba ya

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

heshima kama hii kwamba mtu ana miaka 23 ilhali ana mshichana ambaye anaenda kufunga harusi. Kwa hivyo, nafikiri pengine yale ambayo yalisemwa na mheshimiwa Mazungu pengine yapo na yanamkumba yeye.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Kadenge, what do you have to say about the issues raised by the hon. Members as you also conclude your contribution?

Hon. Kadenge: Nafikiri nimesema ya kuwa nitaleta ushahidi wa kuwa mimi bado nina hiyo miaka 23. Nafikiri ningeliomba mniruhusu niendelee kuunga mkono hii hoja.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Members, just for us to be guided, since he insists that he is 23 years of age, he has an opportunity as he clearly says that he is going to produce a document to still give evidence of the age that he is giving. Failure to do so, then we shall have an avenue that we are going to use for further communication.

Hon. Kadenge: Asante Bw. Spika, but let me withdraw the age limit then...

(Laughter)

Kwa hivyo, ninaendelea kupongeza hii Hoja. Kama mnavyojua sisi wa mijini...

(Hon. Mwarandu stood on a Point of Order)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Mwarandu, you have already stood yet you have not been given an opportunity, you do not have to stand. Proceed. What is your point of order?

Hon. Mwarandu: Mheshimiwa Spika, nashukuru vile ambavyo Mheshimiwa Kadenge amesema kwamba ametoa ile fikira yake kwamba ana miaka 23 lakini atuambie ili tuhakikishe kwamba ana miaka mingapi.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Members, I wish that we are guided by the Motion that is before us as we make our contributions. Let us not bring other issues that may deviate the attention of Members. Please proceed.

Hon. Kadenge: Asante Bw. Spika kwa kunitetea. Hoja hii ikipitishwa hapa itakuwa na umuhimu mkubwa kwa sababu sisi wa mijini tuna shida ya mihadarati. Watoto wetu hawana shughuli za kufanya kwa hivyo tukipata jambo kama hili itakuwa ya msaada mkubwa sana kwa watoto wetu. Nikiangalia ile sehemu iliyowekwa maadhari yake, Magarini Bomani, ni mahali ambapo kuna utulivu. Watoto wetu wa mijini wanaweza kukaa vizuri na kuwa vijana ambao tutawatumia baada ya sisi kustaafu. Tuko na vipaji vingi sana ambavyo tumekuwa tukivikuza na wengi wetu tumekuwa tukiwachangia kuwapeleka uzunguni ili kupata maarifa ambayo tukiwa na hii *academy* hapa Magarini, tutakuwa tumezuia hata kutumia pesa nyingi kuwasafirisha na pia tutakuwa tumesaidika. Huu ni msaada mkubwa kwa Kaunti ya Kilifi. Ninaunga mkono mia kwa mia.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes hon. Changawa.

Hon. Changawa: Asante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nasafi hii. Nimesimama kuunga mkono Hoja ambayo iko mbele ya Bunge hili. Nataka niseme ya kwamba kila mmoja ana fahamu kwamba mtaala wa elimu umebadilika. Mtaala ambao tuko nao saa hii unazingatia upande wa vipaji vya watoto; maswala ya elimu na stakabadhi kufikia saa hii imefika mwisho. Hii ina maana kwamba kama basi mtaala wa elimu unazingatia vipaji vya watoto wetu, ni muhimu Kaunti yetu kuwa na mahali kwa mafunzo kwa watoto wetu. Nikiwa mzazi wa watoto

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wawili saa hii, nitakapojua vipaji vyao mapema nitakuwa na nafasi nzuri kujua ni wapi wanangu wanaweza kukuza talanta zao.

Tumeshindwa na Kaunti nyingine. Wao wameshafanya mambo haya lakini hapa kwetu hatuna hata mahali popote ambapo tumefanya hivi. Hii isiwe sababu. Pengine tukienda Mombasa tunaona viwanja vingi kwa sababu Gavana wao ni mwanariadha; hapa kwetu Gavana wetu hatujamuona akijihusisha na mambo ya riadha. Hiyo haimaanishi tunaweza sema hatuwezi kuja pamoja na kutengeneza mahali kama hapa. Mheshimiwa mwenzangu aliyeongea kuhusu mambo ya umbali wa mahali ambapo uwanja uko, nataka kusema kwamba wanadamu hufwata rasilimali mahali ipo lakini rasilimali haifwati mtu. Katika maendeleo ya Kaunti, hatuwezi tukaеkeza mahali pamoja; ili mahali kwingine kuendeleo na kuitwe mji ni mambo kama haya yafanyike.

Nimesimama kuunga mkono kwamba jambo hili litekelezwe ili kuona kwamba sisi pia tunaingia katika historia. Nataka kusema kwamba mwenye kula pesa nyingi katika ulimwengu wa michezo ni mchezaji Christiano Ronaldo. Anapata shilingi million 22,707,135 kwa siku ambapo hizi pesa nafikiri kama ni mshahara wa Rais wetu, sijui utakuwa ni wa muda gani. Kupitia kwa mafundisho ya watoto wetu juu ya vipaji vyao, tutakuwa tunaboresha maisha ya watoto wetu baadaye. Wacha tuheshimu kipaji ambacho mwanadamu amepewa kutoka kwa Mungu. Haya mengine hapa duniani ni ya kubambanya, usome upate shahada 20 lakini mwisho wa yote, zile shahada ndizo ambazo zimeharibu maisha katika Kaunti hii na Kenya kwa jumla.

Nasema tuheshimu kipawa ambacho mtu amepewa kutoka juu mbinguni. Hayo ni kupitia kwa viwanja kama hivi kujengwa ili tuwafundishe watoto wetu wakiwa wadogo na watakapokuwa wakubwa wawe wa manufaa katika maisha ya baadaye humu nchini.

Nasimama kuunga mkono kwamba kiwanja hiki ikiwezekana kama kinaweza kutengenezwa ndani ya huu muda mchache kabla ya kuanza mwaka wa kifedha wa 20018/2019 kiwe kimeisha, ningefurahi sana. Mimi mwenyewe hucheza michezo ya kuigiza na pia ni mwanariadha lakini kwa sababu ya umri na hatokukuzwa hapo nyumbani katika hizi *sports academy*, basi kama yalikoseka zamani...

(Hon. Changawa spoke off record)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you very much hon. Members for making your contributions regarding the Motion that is before the Floor of the House. Before I put the Question, I would wish to call upon the Mover of the Motion to make his final submissions taking in to consideration the questions and concerns that have been raised by Members. Proceed please.

(Question, that the Mover of the Motion be now called upon to reply, put and agreed to)

Hon. Hadad: Thank you Mr. Speaker. For me to bring such a Motion to the House I had taken some factors into consideration and some of the factors are availability of land, conducive environment and expenses. Since we will not be purchasing the land, job opportunities such as coaches, cleaners, child care doctors will be available. I think hon. Mwarandu mentioned security; we will also be able to employ security guards and this will also be a place where talents will be nurtured and through this, we will be able to empower the youth.

Hon. (Ms) Carol talked about conducting a survey. Before I brought this Motion and gave a specific location, be sure we have already done our own survey and this place is suitable

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

enough for this project. There is something called balancing resources. We cannot bring everything into town; we want Kilifi to grow as a whole...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Mwarandu, you have a point of order, what is your point of Order?

Hon. Mwarandu: The hon. Member is saying that they did their survey. Can he give us a document to show that they really did the survey?

Hon. Hadad: No, survey can mean a lot of things concerning this situation even for you to be given a title deed of the land, there must be a survey of the land so for sure you will receive one. Worry less. So there is balancing of resources. We want Kilifi to grow as a whole not just in partial places. For this Sports Academy to be built in such an area it will bring about urbanization of that area because for it to be accessible, there must be infrastructure; roads, water e.t.c. All must be available for this Sports Academy to be authentic and conducive for everyone.

So without much, I would urge my fellow Members to approve this Motion and let the work begin. If we waste more time, it is not anyone being affected rather than us the youth. So let us not waste time on such matters and let us take a step ahead. Thank you, Mr. Speaker.

(Question proposed)

(Question put and agreed to)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Members, there being no other business, this House stands adjourned until Monday, 26th of March, 2018. Thank you.

The House rose at 3:40 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*